

Jamhuri ya Kiarabu ya Misri  
Tarehe 5 Mwezi Rajab 1444 Hijry  
Wizara ya Waqfu  
27 Januari 2023

(١)

الوطنية بين الحقيقة والادعاء

**Uzalendo kati ya Uhakika na Madai  
Imefasiriwa  
Na  
Profesa Ayman Alasar  
kitivo cha lugha na ufasiri  
Chuo kikuu cha Al Azhar**

Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu Bwana wa viumbe, asemae ndani ya kitabu chake kitukufu: {**Na shikamaneni kwa Kamba ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarikiane**} na ninakiri kwamba hapana mola apasae kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu, hali ya kuwa peke yake hana mshirika, na ninakiri kwamba bwana wetu na Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu shusha rehma, amani na baraka kwa Mtume na jamaa zake na maswahaba zake, na mwenye kuwafuata kwa wema mpaa siku ya malipo. Ama baada ya hayo:

Mwenyezi Mungu Mtukufu ameweza maumbile ya watu kupenda nchi zao, na kuwafanya kujinasibisha nazo na kuzilinda kwa mapenzi ya miyo yao, na Mtume wetu (S.A.W) anatupa mfano wa juu katika kupenda nchi na kuihurumia aliposema akiambia nchi yake ya tukufu ya Makkah: (Naapa kwa Mwenyezi Mungu hakika wewe ndio ardhi bora ya Mwenyezi Mungu, na Ardhi ya Mwenyezi Mungu inayompendeza zaidi, na lau kama nisingefukuzwa katika ardhi yako, nisingetoka).

Vilele Mtume (S.A.W) alipohamia Madina na ikawa nchi yake na mswahaba zake, hakuisahau nchi yake aliyokulia wala nchi

(۲)

yake aliyofikia, akasema Mtume (S.A.W): (Ewe Mwenyezi Mungu tupe mapenzi na Madina kama tunavyoipenda Makkah au zaidi, ewe Mwenyezi Mungu tubariki katika pishi zetu na vibaba vyetu (pishi na vibaba ni vipimo vya watu wazamani).

Na uzalendo wa kweli si kaulimbiu, wala maneno tu, bali ni mapenzi ya kweli, kujitolea na kuwa tayari kujitolea kwa ajili ya nchi, sawasawa kujitoa huko kuwe kwa mali, muda, juhudu au nafsi. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {**Hakika Mwenyezi Mungu amenunua kwa Waumini nafsi zao na mali zao kwa kuwa wao watapata Pepo. Wanapigana katika Njia ya Mwenyezi Mungu - wanauwa na wanauwawa.** Hii ni ahadi aliyo jilazimisha kwa Haki katika Taurati na Injili na Qur'ani. Na nani atimizae ahadi kuliko Mwenyezi Mungu? Basi furahini kwa biashara yenu mliyo fanya naye. Na huko ndiko kufuzu kukubwa} na anasema Mtume (S.A.W): ( Mwenye kuuwawa kwa sababu ya mali yake basi huyo ni shahidi, na mwenye kuuwawa kwa sababu ya jamaa zake basi huyo ni shahidi).

Na Mtume (S.A.W) amewapa bishara walini wa nchi ambao wanajitolea nafsi zao kwa ajili ya kuilinda kikamilifu, anasema Mtume (S.A.W): (Macho mawili hayaguswi na moto, jicho lililolia kwa ajili ya kumuogopa Mwenyezi Mungu, na jicho lililokesha linalolinda katika njia ya Mwenyezi Mungu), na anaseme Mtume (S.A.W): (je, niwajulisheni usiku uliobora zaidi kuliko usiku wa Laylatulqdri? Ni mlinzi anaelinda katika ardhi na hofu huenda asirudi kwa jamaa zake).

Halkadhalika uzalendo wa kweli unahitaji mshikamano na kuhurumiana kati ya raia, na kushirikiana vizuri katika kusaidi mahitaji ya wanyonge na masikini, na kutotumia azma kama fursa

(۳)

ya kufanya biashara, Mwanyezi Mungu Mtukufu anasema: {**Na saidianeni katika wema na uchamngu. Wala msisaidiane katika dhambi na uadui. Na mcheni Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mkali wa kuadhibu.**} na anasema Mtume (S.A.W): (Mtu anaependeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni yule anaewafaa watu, na amali ainayopendeza zaidi kwa Mwenyezi Mungu ni ile furaha unayoingiza kwa Muislamu au kumuondoshea tatizo, au kumlipia deni au kumuondoshea njaa), na anasema Mtume (S.A.W):(Kufanya mambo mema ni kinga ya matatizo, na sadaka ya siri huzima ghadhabu za Mwenyezi Mungu, na kuunga udugu huzidisha baraka ya umri), na anasema Mtume (S.A.W):(Hakika kacula la Ashaaira wakiingia katika vita, au wakipungukiwa na chakula, hukusanya walicho nacho sehemu moja kisha hugawana katika chombo kimoja sawa sawa, basi wao ni mimi na mimi ni mionganoni mwao).

Na mionganoni mwa misingi ya uzalendo ni kufanya kazi na uzalishaji kwa ufanisi na viwango bora kwa makusudio ya kuinua nchi na kuiendeleza, na kwa kufuata amri ya kauli ya Mtume (S.A.W) aliposema: (Hakika Mwenyezi Mungu anapenda mmoja wenu akiifanya kazi, basi aifanye kwa ufanisi), na pia kuhisi usimamizi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa mwanadamu katika harakati zake zote, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Naye yu pamoja nanyi popote mlipo.**} anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu: {**Na huwi katika jambo lolote, wala husomi sehemu yoyote katika Qur'ani, wala hamtendi kitendo chochote ila Sisi huwa ni mashahidi juu yenu mnapo shughulika nayo. Na hakifichikani kwa Mola wako Mlezi chenye uzito hata wa chembe katika ardhi na katika mbingu, wala kidogo kuliko hicho wala kikubwa ila kimo katika Kitabu kilicho wazi.**}

(ε)

\*\*\*

Sifa njema ni za Mwenyezi Mungu, na rehma na amani zimuendaa Mtume na Nabii wa Mwisho, bwana wetu Muhammad (S.A.W), na ali zake na swahaba zake wote.

Na tunasisitiza kuwa uzalendo wa kweli unahitaji kuheshimu bendera ya nchi, wimbo wa taifa, nembo zake na alama zake zote, na kuiwakilisha vizuri ndani na nje na katika mahfali zote za kitaifa na kimataifa, na kuwa na pupa ya kunyanya juu bendera yake, na kupambana na changamoto na hatari zinazoikabili au uzushi, na kuzindika na vitimbi vyta wapinzani wake, na kutokaa jirani na wanaoisema vibaya, bali saidia kuitetea kubainisha uongo wa wanaoisema vibaya.

Mzalendo wa kweli haongopi, hasaliti, haghushi, hafichi bidhaa wala hali njama na kusambaza uzushi, uzalendo wa kweli ni kujenga si kubomoa, uzalendo wa kweli ni sanaa ya kutengeneza maisha na kuendeleza Dunia, Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: {**Yeye ndiye aliye kuumbeni katika ardhi, na akakuwekeni humo.**} popote panapokuwa maslahi na ujenzi basi panakuwa na sharia ya Mwenyezi Mungu na uislamu sahihi na uzalendo wa kweli, na popote panapokuwa na uharibifu na kutumia azma kama sehemu ya biashara basi hapo kuna madai ya uongo na uzalendo bandia.

Ewe Mwenyezi Mungu ilinde Misri yetu na inyanyue bendera yake Ulimwenguni.